**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**


Ofisi ya Mkurugenzi Mtendajji (W),
*S.L.P. 20,*
***MISUNGWI***

*Simu: 255-732980745*
*Fax: 255 732980745*


---

Kumb.Na. MZA/MDC/S.10/35/43 16/05/2018

Kwa Wananchi wote,

**YAH: TANGAZO LA KAZI**
**(NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA KWA KADA ZA AFYA)**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo ya Afya, Shirika la AGPAHI anawatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba kujaza jumla ya nafasi 24 za ajira kwa kada mbalimbali katika vituo 12 vya kutolea huduma za Afya.

**1.0: AFISA TABIBU (CLINICAL OFFICER) II - NAFASI 6**

**1.1: Sifa Mahsusi za Muombaji.**
Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya Utabibu (Clinical Medicine) ngazi ya Stashahada (Diploma) katika Chuo kinachotambulika na Serikali.

**1.2: Kazi na Majukumu**
1) Kutambua na kutibu wagonjwa wa kawaida.
2) Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake.
3) Kufanya upasuaji mdogo.
4) Kushiriki kupanga na kutekeleza huduma za afya ya msingi.
5) Kuelimisha jamii na kutoa ushauri nasaha kwa wagonjwa.
6) Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za Afya na mfuko wa Afya ya Jamii.
7) Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma.
8) Kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za kituo.
9) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

## 2.0: AFISA MUUGUZI MSAIDIZI (ANO) II - NAFASI 2

### 2:1: Sifa Mahsusi za Muombaji.

Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya Uuguzi na Ukunga (Nursing and Midwifey training) ngazi ya Stashahada (Diploma) katika Chuo kinachotambulika na Serikali na kusajiliwa (registered) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

### 2.2: Kazi na Majukumu.

1) Kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga.
2) Kukusanya takwimu muhimu za Afya.
3) Kuwaelekeza kazi Watumishi, Wauguzi walio chini yake.
4) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya.
5) Kutoa huduma za kinga, tiba, afya ya uzazi na mtoto.
6) Kutoa huduma za wagonjwa majumbani na kutoa ushauri nasaha katika matatizo kwa mtu binafsi au familia husika.
7) Kuelekeza na kusimamia mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi.
8) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

## 3.0: MUUGUZI (NURSE) II - NAFASI 8

### 3:1: Sifa Mahsusi za Muombaji.

Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya Uuguzi na Ukunga (Nursing and Midwifey training) ngazi ya Astashahada (Certificate) katika Chuo kinachotambulika na Serikali na kusajiliwa (registered) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

### 3.2: Kazi na Majukumu.

1) Kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga.
2) Kukusanya takwimu muhimu za Afya.
3) Kuwaelekeza kazi Watumishi, Wauguzi walio chini yake.
4) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya.
5) Kutoa huduma za kinga, tiba, afya ya uzazi na mtoto.
6) Kutoa huduma za wagonjwa majumbani na kutoa ushauri nasaha katika matatizo kwa mtu binafsi au familia husika.
7) Kuelekeza na kusimamia mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi.
8) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

## 4.0: MTEKNOLOJIA (MAABARA) II - NAFASI 7

### 4.1: Sifa Mahsusi za Muombaji.

Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya sayanzi za maabara za afya (health laboratory science) ngazi ya Stashahada (Diploma) katika chuo kinachotambulika na Serikali.

### 4.2: Kazi na Majukumu.

1) Kupima sampuli zinazoletwa Maabara.
2) Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa Maabara za ngazi za juu.
3) Kuhifadhi na kufanya ukaguzi wa vitendanishi, vifaa, kemikali katika Maabara.
4) Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma.
5) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

## 5.0: DAKTARI MSAIDIZI (AMO) - NAFASI 1

### 5:1: Sifa Mahsusi za Muombaji.

Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya ngazi ya Stashahada ya juu ya Udaktari katika Chuo kinachotambulika na Serikali.

### 1.2: Kazi na Majukumu

1) Kutambua matatizo ya wagonjwa na kutoa huduma za tiba, kinga na huduma kwa kina mama na mtoto.
2) Kufanya upasuaji wa dharura na wa kawaida.
3) Kupanga, kutekeleza na kutathmini huduma za afya sehemu za kazi.
4) Kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ya afya ili kuboresha utoaji wa huduma.
5) Kupanga utekelezaji wa mipango ya kukabili majanga na dharura mbalimbali za wagonjwa.
6) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

## 6.0: SIFA ZA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

1) Awe ni raia wa Tanzania.
2) Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na si zaidi ya miaka 45.
3) Awe na elimu ya sekondari na cheti cha taaluma cha kidato cha sita/ au kidato cha nne.
4) Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo stahili ya nafasi anayoomba.
5) Awe na uwezo wa kutunza siri za wateja anaowahudumia.
6) Awe tayari kufanya kazi na kuishi katika mazingira yoyote hasa vijijini.

Ajira hizi ni za mkataba wa miezi mitano (5) ambao unaweza kuhuishwa (renewable) baada ya kipindi hicho kuisha ukiwa umetumikia kwa weledi na ufanisi. Waombaji watakaofaulu zoezi la usaili watapangiwa kufanya kazi katika Kituo/Zahanati za Mwawile Disp, Kolomije H/C, Mbarika H/C, Misungwi Hosp, Mwamboku Disp, Igokelo Disp, Nyahiti Disp, Bugisha Disp, Nyamijundu Disp, Mwanangwa Disp, Mondo Disp, Igongwa Disp, MisasiH/C, Buhingo Disp, Sumbugu Disp na Buhunda Disp.

7. **JINSI YA KUOMBA**

Barua ya maombi iandikwe kwa mkono ukiambatisha CV na nakala za vyeti vyote vya taaluma na ujuzi, cheti cha kuzaliwa. Pia ambatisha picha mbili za hivi karibuni (ppt size).

Barua zote za maombi zitumwe kwa kuwasilisha mwenyewe mkononi Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Misungwi au kutumwa kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)<br>
Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi<br>
S.L.P. 20,<br>
**MISUNGWI.**

8. **MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI**

Siku ya mwisho ya kupokea maombi ni jumatatu tarehe **22 Mei 2018** saa **9:30 Alasiri**.

E.L. Mwaiteleke<br>
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**<br>
**MISUNGWI**

MKURUGENZI MTENDAJI<br>
HALMASHAURI YA WILAYA<br>
MISUNGWI